MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

**Na: 11. Msimu wa Kilimo 2019/20 Tathmini Januari 11-30, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Januari 21-31, 2020**

**Muhtasari**

- Vipindi vya mvua za nje ya msimu zinazotarajiwa kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua zinaweza kuathiri mazao yaliyokomaa hata hivyo zitasaidia mazao yaliyochelewa kupandwa.
- Kwa maeneo ambako kunatarajiwa kuwa na vipindi vifupi vya upepo mkali, wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani na kufuatilia taarifa za hali ya hewa.


## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2020

Katika dikadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini(St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu. Hali hii ilisababisha ukanda wa mvua kubaki kusini mwa nchi yetu. Joto la bahari la juu ya wastani liliojitok

eza katika maeneo ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hali lilisanbabisha kutokea kwa vipindi vifupi vya migandamizo midogo ya hewa. Katika eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) Joto la bahari lilikuwa la wastani. Hali hii ilipelekea uwepo wa upepo hafifu kuvuma kutoka magharibi hivyo kuwa na mchango mdogo katika kuimarisha mifumo ya unyevunyevu kutoka katika misitu ya Congo kuja katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2020

Katika kipindi cha Novemba 21-30, 2019, maeneo mengi ya nchi yalipata mvua. Kiasi cha mvua cha zaidi ya milimita 100 kilipatikana katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Kwa maeneo machache ya kusini magharibi ya mkoa wa Morogoro yamepata kiasi cha mvua zaidi ya milimita 250 kama inavyoonekana katika kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Januari 11- 20, 2020

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2020

Katika kipindi hiki, kiwango cha mvua kilicho rekodiwa kilisaidia ukuaji wa mazao hasusan katika ukanda unaopata mvua msimu moja kwa mwaka hususan Iringa, Mbeya, Njombe, Rukwa, Tabora and Kigoma wakulima waliendelea na palizi la mahindi. Mikoa ya Singida, Dodoma, Lindi na Mtwara mazao ya mahindi , alizeti na ngano yalikuwa katika hatua ya jani la tatu. Maeneo mengi ya ukanda unaopata mvua mbili kwa mwaka wakulima waliendelea na shughuli za palizi na uvunaji. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya mikoa ya Mara, Shinyanga, Simiyu, Kilimanjaro, Arusha and Manyara zao la mahindi lilikuwa katika hatua kati ya jani la tisa na kukomaa.Katika mkoa wa Kagera wakulima walijihusisha na uvunaji wa mahindi na maharagwe.

Kutokana na kuwepo kwa wadudu waharibifu dumuzi katika mkoa wa Tabora na Viwavijeshe kwa upande wa Simiyu wakulima waliendelea na upuliziaji wa madawa ya kuulia wadudu.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2020

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito vimeanza kuongozeka katika maeneo mbalimbali ya nchi kutokana na mvua zinazoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31, 2020.

Katika dikadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha ukanda wa mvua kubaki kusini katika nchi yetu. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea kuonekana katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hali inayotarajiwa kusababisha kutokea kwa vimbunga. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na kupelekea upepo hafifu kuvuma kutoka magharibi hivyo kuwa na mchango mdogo katika kuimarisha mifumo ya unyevunyevu kutoka katika misitu ya Congo kuja katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu.

## HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31, 2020.

Maeneo ya Kanda ya Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajiwa kupata mvua katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) kunatarajwa kuwa na vipindi vya mvua za wastani katika maeneo machache hususani katika siku tano za mwanzo za dikadi hii.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) kunatarajiwa kupata mvua za wastani katika maeneo machache na vipindi vifupi vya upepo mkali.

Nyanda za juu Kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na Kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kupata mvua za wastani katika baadhi ya maeneo pamoja na vipindi vifupi vya upepo mkali.

## HALI YA HEWA KILIMO INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31,2020.

Mvua zinazotarajiwa katika maeneo mengi ya nchi zitasaidia utunzaji wa unyevunyevu kwenye ardhi kwa ajili ya mazao na malisho hasa katika ukanda wa mvua msimu mmoja kwa mwaka. Katika ukanda unaopata mvua misimu miwili kwa mwaka, wakulima wanashauriwa kuendelea na uandaaji wa mashamba na palizi. Kwa maeneo ambayo mazao yameathiriwa na wadudu, wakulima wanashauriwa kupata ushauri wa kitaalam ili kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea. Hata hivyo, wakulima na wafugaji wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa ugani kwa ajili ya maelekezo juu ya utumiaji wa pembejeo za kilimo na kufuatilia taarifa za hali ya hewa zinazotolewa, ambazo nyingine hupatikana kwenye tovuti ya TMA (http://ww w.meteo.go.tz/).

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2020

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka kiasi katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka hususan bonde la maji la Ziwa Viktoria, Rufiji, Pangani na Wami/Ruvu. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuendelea kuyatumia kwa uangalifu.

*Jarida limetayarishwa na:*

**Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**
**Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro,** Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***